

# UNACHOTAKIWA KUJUA KUHUSU CHANJO ZA VIRUSI VYA COVID-19

Januari 26, 2021

Chanjo za COVID-19 hatimaye zitatolewa kwa watu wazima wanaoishi Canada. Picha hizi za maelezo ni za kwanza katika mfululizo ulioundwa kukupa maelezo ya matibabu ambayo ni sahihi na yaliyothibitishwa, kuhusu chanjo hizi ili uweze kufanya maamuzi sahihi.

## Ujumbe Muhimu:

- Chanjo ya COVID-19 itasaidia kukuinga dhidi ya kuambukizwa COVID-19. Dozi mbili zinahitajika.
- Chanjo za COVID-19 zimefanyiwa tafiti kubwa za kisayansi na majaribio kwa kina katika aina mbalimbali za watu na zinaaminika kuwa salama na zenye ufanisi mkubwa.

## Kwa nini Upate Chanjo ya COVID-19?

- Kwa miaka mingi, watu kote ulimwenguni wametumia chanjo kujikinga dhidi ya magonjwa hatari ya kuambukiza, kama vile surua, pepopunda na polio.
- Chanjo ya COVID-19 ndiyo njia bora zaidi ya kujikinga dhidi ya kuambukizwa COVID-19 na pia kutusaidia ili kila mtu arudi kuendeleza maisha kama kawaida.
- Chanjo ni njia kuu ya kuzuia kuenea kwa virusi hivi katika familia na jamii zetu, kando na kuvaa barakoa, kunawa mikono na kukaa angalau mita 2 mbali na wengine.

## Je, Chanjo Hufanya Kazi Vipi?

- Chanjo haziponyi, bali zinasaidia kuwakinga watu wasiugue.
- Chanjo huufundisha mwili wako mwonekano wa virusi vya COVID-19 ili mwili wako uweze kuvitambua na kupambana na virusi ikiwa utaambukizwa navyo.
- Chanjo ya COVID-19 hufanya hivi kwa kutuma maagizo ("mRNA") kwa mwili wako ili mwili wako utengeneze protini zenye ncha kama zile zilizo kwenye sehemu ya juu ya virusi vya COVID-19. Protini hizi hazikuambukizi ugonjwa. Mfumo wako wa kinga mwilini kisha hutengeneza fungomwili za kupambana na maambukizi ikiwa virusi vya COVID-19 vitaingia mwilini siku za baadaye.

## Chanjo Zina Ufanisi Gani?

- Kufikia sasa, chanjo mbili zinatolewa nchini Canada, moja inatolewa na Pfizer/BioNTech na nyingine inatolewa na Moderna.
- Chanjo zote mbili zinaaminika kuwa fanisi sana katika kuzuia ugonjwa wa COVID-19 baada ya dozi mbili. Zimegunduliwa kuwa na ufanisi wa asilimia tisini na tano (95%) katika tafiti kubwa za kisayansi.



## Je, Athari za Chanjo Hizi ni Gani?

Chanjo za COVID-19 zinaaminika kuwa salama kabisa. Kwa ujumla, athari zilizotambuliwa katika tafiti za kisayansi za chanjo za COVID-19 ni sawa na zile zinazoweza kutokea kutokana na chanjo zingine. Athari hizi zilijumuisha mambo kama maumivu ya bega/mkono mahali palipochomwa sindano, maumivu ya mwili na misuli, kuhisi baridi, uchovu na homa. Hizi ni athari za kawaida za chanjo na hazina hatari kubwa ya afya. Athari hizi zikitokea, kawaida zitakwisha baada ya siku moja hivi. Dalili hizi zinaweza kutokea baada ya dozi zote mbili za chanjo hii.

Kama chanjo zote zilivyo, kuna uwezekano mdogo sana wa athari mbaya zaidi kutokea, kama vile mzio (au alaji). Ndiyo sababu utaombwa kukaa katika kituo cha chanjo (kliniki au ofisi ya daktari wako) kwa dakika 15-30 baada ya kuchanjwa, ili wahudumu wa kimatibabu waweze kukuhudumia.

## Chanjo haiwezi kukuambukiza ugonjwa wa COVID-19.

### Ninaweza Kupata Wapi Maelezo Zaidi?

Serikali ya Canada pia imekagua kwa uangalifu ushahidi uliopo wa kimatibabu na hakuna wasiwasi wowote mkubwa wa usalama uliotambuliwa. Muhtasari wa Health Canada wa chanjo ya Pfizer BioNTech na Moderna kwa Kiingereza na Kifaransa unapatikana hapa:

<https://www.canada.ca/en/health-canada/services/drugs-health-products/covid19-industry/drugs-vaccines-treatments/vaccines/pfizer-biontech.html>

<https://www.canada.ca/en/health-canada/services/drugs-health-products/covid19-industry/drugs-vaccines-treatments/vaccines/moderna.html>

Maelezo yaliyo katika hati hii yamethibitishwa na madaktari wa Canada: Meb Rashid MD, Profesa Msaidizi, Chuo Kikuu cha Toronto, Vanessa Redditt, MD, Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Toronto na Isaac I. Bogoch, MD, Profesa Mshirika, Chuo Kikuu cha Toronto

